JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2016

# MAELEZO YA WAZIRI

Tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya limeendelea kuiathiri nchi yetu. Bangi imeendelea kuwa ni dawa ya kulevya inayotumika zaidi na ikizalishwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara hususani katika mikoa ya Mara, Morogoro, Arusha, Tanga, Mbeya, Kagera, Ruvuma, Iringa na Njombe.
Vilevile, Mirungi imeendelea kutumika na kuzalishwa hapa nchini hasa katika Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Same na kiasi kingine cha dawa hii kimekuwa kikiingizwa nchini kutoka nchi jirani ya Kenya.


Nchi yetu imekuwa ni njia kuu ya kupitishia na kusambaza dawa za kulevya za viwandani hususan heroin na cocaine kwenda Ulaya, China, Afrika Magharibi na Afrika Kusini na kiasi kingine kubaki na kutumika hapa nchini. Kiasi kikubwa cha Heroin inayoingizwa nchini hutokea nchi za Afghanistan, Pakistan na Iran wakati kiasi kikubwa cha cocaine hutoka nchi za Amerika ya Kusini hasa Colombia, Peru na Bolivia.

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya limeendelea kuathiri sekta mbalimbali za uzalishaji na hivyo kudhoofisha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Matumizi hayo yamekuwa yakiathiri afya za watanzania hasa vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa letu.

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi imefanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya athari za matumizi na biashara ya dawa za kulevya, kutoa matibabu kwa wanaotumia dawa za kulevya na kudhibiti uingizaji na usambazaji wa dawa hizo hapa nchini. Jitihada nyingine zilizofanywa na Serikali kwa mwaka 2016 ni kukamilisha rasimu ya kwanza ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015.

Udhibiti wa tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya unakabiliwa na changamoto mbalimbali, changamoto hizo ni pamoja na; kuongezeka kwa kasi kwa wanaohitaji huduma za tiba ya uraibu na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hizi, uhitaji mkubwa wa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya, uzalishaji wa dawa mpya za kulevya kwa kutumia kemikali bashirifu, matumizi mabaya ya dawa za tiba zenye asili ya kulevya,ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi na kubadilika mara kwa mara kwa mbinu zinazotumika kuingiza na kusambaza dawa za kulevya nchini (concealment methods).

Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza wadau wote kwa kutoa ushirikiano katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevyanchini. Tatizo hili ni mtambuka hivyo linahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali wa sekta tofauti. Vilevile, naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba wadau wote kushiriki kwa dhati kabisa katika kukabiliana na tatizo hili la matumizi na biashara ya dawa za kulevya.



Jenista Joakim Mhagama (Mb)
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu**
**(Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu)**

# DIBAJI


Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini ya mwaka 2016 imeandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Na. 5 ya mwaka 2015, kifungu cha 60. Dhumuni la taarifa hii nikuonesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na kuifahamisha jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya lilivyokuwa nchini kwa mwaka 2016 pamoja na jitihada, mafanikio, matatizo na changamoto zilizojitokeza.

Taarifa hii husaidia kuongeza uelewa wa jamii kuhusu tatizo la dawa za kulevya na kuonesha changamoto zilizopo kwenye udhibiti wake ili wadau mbalimbali, wakiwemo wananchi, waweze kushiriki na kuimarisha mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Taarifa hii imeandaliwa kwa kutumia takwimu na taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali katika udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya nchini. Vilevile, imejumuisha taarifa kutoka mashirika ya kimataifa ikiwemo Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za kulevya na Uhalifu (UNODC) na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawaza Kulevya (INCB).

Taarifa hii imegawanyika katika sura nne. Sura ya Kwanza inaelezea tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya lilivyo nchini kwa mwaka 2016, zikiwemo mbinu zinazotumiwa kuingiza na kuzisambaza dawa hizi nchini na kuzisafirisha nje ya nchi. Sura ya Pili inaelezea mwenendo wa tatizo la dawa za kulevya duniani pamoja na jitihada zilizofanyika katika mabara na nchi mbalimbali. Sura ya Tatu imejikita kwenye kuelezea udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini. Sura ya Nne inakamilisha taarifa hii kwa kuonesha matatizo na changamoto zilizojitokeza katika udhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya nchini kwa mwaka 2016.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliowasilisha taarifa kutoka kwenye maeneo yao ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangia kufanikisha uandaaji wa taarifa hii. Vilevile, kwa wale ambao kwa namna moja ama nyingine walishindwa kuwasilisha taarifa zao naomba wajitahidi wakati ujao waweze kuwasilisha kwa wakati ili kufanikisha uandaaji wa taarifa yenye tija.



Rogers William Siyanga
**Kamishna Jenerali**
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

# YALIYOMO

MAELEZO YA WAZIRI........................................................................................ i
DIBAJI.................................................................................................................. iii
YALIYOMO.......................................................................................................... iv
VIFUPISHO.......................................................................................................... vi
SURA YA KWANZA............................................................................................. 1
1 TATIZO LA MATUMIZI NA BIASHARA YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI.............................................................................................................. 1
1.1 Biashara ya Dawa za Kulevya.................................................... 1
1.2 Mwenendo wa Biashara ya Dawa za Kulevya Nchini.............. 2
1.2.1 Bangi................................................................................................ 2
1.2.2 Mirungi............................................................................................. 2
1.2.3 Heroin............................................................................................... 5
1.2.4 Cocaine............................................................................................. 5
1.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya................................................... 7
1.3.1 Watumiaji na Sababu za Matumizi ya Dawa za Kulevya.......... 7
1.3.2 Maeneo ya Utumiaji..................................................................... 8
1.4 Madhara ya Dawa za Kulevya.................................................... 8
1.4.1 Kiafya................................................................................................ 8
1.4.2 Kijamii.............................................................................................. 9
1.4.3 Kiusalama........................................................................................ 9
1.4.4 Kiuchumi......................................................................................... 9
1.4.5 Kisiasa.............................................................................................. 10
1.4.6 Kimazingira..................................................................................... 10
SURA YA PILI...................................................................................................... 12
2 MWENENDO WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI.. 12
2.1 AFRIKA............................................................................................ 12
2.2 ULAYA.............................................................................................. 13
2.3 ASIA.................................................................................................. 13
2.3.1 Mashariki na Kusini – mashariki mwa Asia............................. 13
2.3.2 Asia Kusini....................................................................................... 16
2.3.3 Asia Magharibi................................................................................ 17
2.4 AMERIKA......................................................................................... 18
2.4.1 Amerika ya Kati na Caribbean.................................................... 18
2.4.2 Amerika ya Kaskazini................................................................... 19
2.4.3 Amerika ya Kusini.......................................................................... 21
2.5 OCEANIA......................................................................................... 22

SURA YA TATU........................................................................................ 26
3 UDHIBITI NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI........................................................................................ 26
3.1 Mapambano Dhidi ya Upatikanaji wa Dawa za Kulevya......... 26
3.1.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu................................................... 26
3.1.2 Udhibiti wa Dawa za Tiba zenye Asili ya Kulevya.................... 27
3.1.3 Kesi za Dawa za Kulevya............................................................. 29
3.1.4 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya................................................. 29
3.2 Kinga na Tiba........................................................................... 29
3.2.1 Elimu kwa Umma......................................................................... 30
3.2.2 Tiba ya Methadone....................................................................... 30
SURA YA NNE........................................................................................ 35
4 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE.............................. 35
4.1 Changamoto.............................................................................. 35
4.2 Hatua za Kukabiliana na Changamoto....................................... 36

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AMKUDAKU | Amua Kuacha Dawa za Kulevya |
| ART | Antiretroviral Therapy |
| ATS | Amphetimine-type Stimulants |
| CDC | Centres for Disease Control and Prevetion |
| CICAD | Inter-American Drug Abuse Control Commission |
| CODATZ | Community Oriented Development Action Tanzania |
| INCB | International Narcotics Control Board |
| LSD | Lysergic Acid Diethylamide |
| MDMA | 3,4-methylene-dioxy-methamphetamine |
| MSD | Medical Stores Department |
| PEDDEREF | People with Drug Dependence Relief Foundation |
| TADERO | Lake Tanganyika Development and Relief Organization |
| TAYOHAG | Tanzania Youth Handcraft Group |
| TB | Tuberculosis |
| TFDA | Tanzania Food and DrugAuthority |
| T-IOGT | Tanzania International Organization of Good Tenplars |
| UAE | United Arab Emirates |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNODC | United Nations Office on Drug and Crime |
| WHO | World Health Organization |
| YAVT | Youth Achievement Village in Tanzania |
| YOVARIBE | Youth Volunteers Against Risky Behaviours |
| VVU | Virusi Vya Ukimwi |

# SURA YA KWANZA

## 1 TATIZO LA MATUMIZI NA BIASHARA YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

Katika kipindi cha mwaka 2016, Tanzania iliendelea kukabiliwa na tatizo kubwa la matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

### 1.1 Biashara ya Dawa za Kulevya

Biashara ya dawa za kulevya huhusisha dawa zinazozalishwa nchini na zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Dawa za kulevya zinazozalishwa nchini ni bangi, mirungi na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi ni pamoja na heroin, cocaine, mandrax, morphine na bangi iliyosindikwa. Mitandao ya kihalifu husafirisha dawa hizi ndani na nje ya nchi kwa njia ya maji, anga na nchi kavu. Mbinu zinazotumika kusafirisha dawa hizo ni pamoja na kuficha kwenye mabegi, kwenye maiti, vinyago, viatu, nywele, sehemu za mwili, kwenye mizigo au bidhaa mbalimbali, kumeza, kutumia makampuni ya usafirishaji vifurushi au kusafirisha kiasi kidogo ambacho si rahisi kugundulika.

Sababu mbalimbali zilichangia kuwepo kwa biashara ya dawa za kulevya nchini ni pamoja na; hali ya hewa inayoruhusu kustawi kwa mimea ya bangi na mirungi, uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi juu ya madhara ya dawa za kulevya, uwepo wa soko la dawa hizo nchini pamoja na kuwepo kwa baadhi ya watu wenye tamaa ya kujipatia utajiri kwa njia yoyote. Sababu nyingine niupungufu wa rasilimali katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kutokana na wingi wa vituo bubu vya kuingilia nchini, ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2016 iliyoandaliwa na UNODC, Tanzania iliendelea kuwa kitovu cha kupitisha heroin kutoka Afghanistan kupitia Iran na Pakistan kwenda Afrika Kusini, nchi za Ulaya na maeneo mengine duniani. Hii inadhihirishwa na kuwepo kwa watanzania waliokamatwa kwa tuhuma za usafirishaji wa dawa za kulevya katikanchi mbalimbali. Licha ya watanzania kujihusisha na biashara hii haramu, wapo pia raia wa kigeni kutoka nchi za Afrika Magharibi kama vile Nigeria na nchi za Asia zikiwemo Pakistan na Iran kukamatwa na kiasi kikubwa cha heroin kwenye Ukanda wa Pwani ya Tanzania mwaka 2016, kunaashiria nchi yetu kuendelea kutumika kupitisha dawa hiyo.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini wa mwaka 2015 uliohusu tathmini ya tatizo la matumizi ya dawa za kulevya katika mikoa 14 ya Tanzania Bara, ulionesha kuwa idadi ya

wafanyabiashara na waathirka wa dawa za kulevya mitaani imeongezeka katika kipindi cha miaka 10 iliyopita na mikoa ya Dar es Salaam na Tanga iliendelea kuwa kitovu cha biashara hiyo

**1.2 Mwenendo wa Biashara ya Dawa za Kulevya Nchini**

Biashara ya dawa za kulevya hufanyika kwa kificho na usiri mkubwa hivyo kuwa vigumu kupata takwimu sahihi za biashara hiyo. Hata hivyo, takwimu za ukamataji, idadi ya watuhumiwa na uteketezaji wa mashamba ya bangi vinaashiria kuwa biashara hii iliendelea kufanyika. Mwenendo wa tatizo la biashara ya dawa za kulevya umeoneshwa hapa chini:-

**1.2.1 Bangi**


Majani ya Bangi


Bangi, Mbegu na Misokoto


Bangi Iliyosindikwa

Biashara ya bangi iliendelea kufanyika kwa kiasi kikubwa mwaka 2016 kama inavyodhihirishwa na kukamatwa kwa tani 68.23 za dawa hiyo kiasi ambacho ni kikubwa kulinganisha na tani 22.01 zilizokamatwa mwaka 2015. Pia, takwimu za ukamataji zinaonesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliojihusisha na biashara ya bangi mwaka 2016 ilikuwa 17,889 ambayo ni kubwa zaidi ikilinganishwa na watuhumiwa 13,275 waliohusishwa na biashara ya dawa hiyo mwaka 2015(Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1).

**1.2.2 Mirungi**


Majani ya Mirungi


Mafungu ya Mirungi



Mafungu ya Mirungi

Mwaka 2016 Biashara ya mirungi iliendelea kufanyika ambapo jumla ya tani 21.64 za dawa hii zilikamatwa. Pia mwaka huo, kulikuwa na watuhumiwa 2,397 waliojihusisha na biashara hiyo, ambayo ni idadi kubwa zaidi ikilinganishwa na idadi ya watuhumiwa katika miaka mingine (Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1).

**Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2006-2016.**

| Mwaka | Kiasi cha Bangi (Tani) | Kiasi cha Mirungi (Kg) |
|---|---|---|
| 2006 | 225.3 | 5144.5 |
| 2007 | 60 | 2164.6 |
| 2008 | 76.4 | 5332.1 |
| 2009 | 56.2 | 22904 |
| 2010 | 4.03 | 3692.4 |
| 2011 | 17.3 | 102 |
| 2012 | 48.7 | 6,216 |
| 2013 | 85.8 | 12,820 |
| 2014 | 81.3 | 15,740 |
| 2015 | 22.01 | 16,599 |
| 2016 | 68.23 | 21,641.12 |

**KielelezoNa.1:MwenendowaKiasichaBanginaMirungikilichokamatwanchini kati ya Mwaka 2006-2016.**





Kielelezo Na.1 kinaonesha kuwa kiasi cha bangi kilichokamatwa kilianza kupungua mwaka 2014na kupungua zaidi mwaka 2015.Mwaka 2016, kiasi cha bangi kilichokamatwa kimeonekana kuanza kuongezeka.

**Jedwali Na.2: Idadi ya watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya mwaka 2006-2016**

| Mwaka | Idadi ya Watuhumiwa – Bangi | Idadi ya Watuhumiwa - Mirungi |
|---|---:|---:|
| 2006 | 6,215 | 574 |
| 2007 | 7,161 | 648 |
| 2008 | 5,670 | 468 |
| 2009 | 3,382 | 365 |
| 2010 | 11 | 26 |
| 2011 | 39 | 100 |
| 2012 | 5,548 | 847 |
| 2013 | 1,547 | 581 |
| 2014 | 11,918 | 1,650 |
| 2015 | 13,275 | 1,780 |
| 2016 | 17,889 | 2,397 |

**Kielelezo na.2: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa kwa kujihusisha na Bangi na Mirungi nchini kati ya Mwaka 2006 - 2016**




Kielelezo Na.2 kinaonesha kuwa katika mwaka 2016 idadi kubwa zaidi ya watuhumiwa walikamatwa wakijihusisha na biashara ya bangi na mirungi.

### 1.2.3 Heroin


Uvunaji wa Opium



Pipi



Kete za Heroin

Mwaka 2016 jumla ya kilo 42 za heroin zilikamatwa nchini zikiwahusisha watuhumiwa 716. Idadi hii ya watuhumiwa ni kubwa ikilinganishwa na watuhumiwa waliokamatwa kati ya kipindi cha mwaka 2006 hadi 2015 (Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.3).

### 1.2.4 Cocaine


Jani la Coca


Cocaine ya Unga


Cocaine ya Mawe


Mwaka 2016 biashara ya cocaine iliendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali nchini. Hii inadhihirishwa na kukamatwa kwa kilo 18.52 za cocaine zikiwahusisha watuhumiwa 263 (Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.3).

Jedwali Na.3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2006-2016.

| Mwaka | Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa(Kg) | Kiasi cha Heroin kilichokamatwa (Kg) |
|---|---:|---:|
| 2006 | 4.13 | 91.7 |
| 2007 | 6.64 | 16.2 |
| 2008 | 3.50 | 3.7 |
| 2009 | 4.39 | 9 |
| 2010 | 62.97 | 185.8 |
| 2011 | 128 | 264.26 |
| 2012 | 151 | 260 |
| 2013 | 4 | 36 |
| 2014 | 45 | 400 |

| | | |
|---|---|---|
| 2015 | 17.79 | 64.75 |
| 2016 | 18.52 | 42.26 |


**Kielelezo Na.3: Mwenendo wa kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2006-2016.**




**Jedwali Na.4: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2006 - 2016.**

| Mwaka | Idadi ya Watuhumiwa wa Cocaine | Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin |
|---|---|---|
| 2006 | 136 | 207 |
| 2007 | 138 | 254 |
| 2008 | 251 | 203 |
| 2009 | 108 | 122 |
| 2010 | 8 | 15 |
| 2011 | 30 | 20 |
| 2012 | 138 | 400 |
| 2013 | 20 | 75 |
| 2014 | 351 | 584 |
| 2015 | 281 | 474 |
| 2016 | 263 | 716 |

**Kielelezo Na.3: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2006 - 2016.**




## 1.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Bangi hutumika kwa wingi nchini ikifuatiwa na heroin, mirungi na cocaine. Watumiaji wa dawa za kulevya pia hutumia dawa za tiba zenye asili ya kulevya kama vile valium, pethidine, tramadol, phenorbabitone na carbamazepine wanapokosa dawa za kulevya walizozizoea. Pia wako baadhi ya watu walioathirika kwa matumizi mabaya ya dawa hizi.

Kulingana na tafiti mbalimbali za mwaka 2014, inakadiriwa kwamba watumiaji wa heroin ni kati ya 250,000 na 420,500 nchini (Consesus Estimate on Key Population Size and HIV Prevalence in Tanzania, 2014). Taarifa zisizo rasmi zinaonesha kwamba waathirika wa dawa za kulevya hasa heroin ni wengi katika maeneo ya mjini hasa Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Tanga, Mbeya na Kilimanjaro.

### 1.3.1 Watumiaji na Sababu za Matumizi ya Dawa za Kulevya

#### 1.3.1.1 Sababu za matumizi ya dawa za kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya hutokana na sababu mbalimbali zikiwemo malezi duni, msukumo rika, kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo, utoro mashuleni na ushawishi kutoka kwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Sababu nyingine ni pamoja na kuvunjika kwa familia, ukosefu wa hofu ya Mungu, msongo wa mawazo, uelewa mdogo juu ya madhara ya dawa hizo, mmomonyoko wa maadili, upungufu wa stadi za maisha na upatikanaji wa dawa za kulevya.

Mitandao ya kijamii imeendelea kuwa chanzo kikubwa cha kuhamasisha matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana walio katika mfumo rasmi wa elimu na wale walio nje ya mfumo wa elimu kutokana na matumizi makubwa ya simu za viganjani zenye mtandao. Kumekuwa na wimbi kubwa la baadhi ya wasanii kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya jambo linalochangia vijana wengi kuhamasika kutumia dawa hizo.

#### 1.3.1.2 Watumiaji wa dawa za kulevya

Kulingana na taarifa ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2015 imeonekana kuwa matumizi ya dawa za kulevya huanzia katika umri mdogo zaidi kati ya miaka 14 - 25. Hata hivyo, taarifa kutoka kliniki za Methadone za Muhimbili, Mwananyamala na Temeke zinaonesha kuwa waathirika wanaohudumiwa katika Kliniki hizo wengine huanza wakiwa na umri mdogo hadi miaka 12. Taarifa hizo pia zinaonesha kuwa baadhi ya watumiaji wa dawa za kulevya wana umri zaidi ya miaka 60.

### 1.3.2 Maeneo ya Utumiaji

Kulingana na taarifa mbalimbali za asasi za kiraia na taasisi za Serikali kwa mwaka 2016, maeneo yaliyoonekana kutumiwa na watumiaji wa dawa za kulevya ni pamoja na vituo vya mabasi, fukwe za bahari, maziwa na mito, mialo ya uvuvi, viwanja vya michezo,kumbi za starehe, na maeneo yaliyopo kando ya barabara kuu. Maeneo mengine ni kwenye majengo yaliyotelekezwa na maeneo ya makazi ya watu wa kipato cha chini.

## 1.4 Madhara ya Dawa za Kulevya

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya vimeendelea kuleta madhara ya kiafya, kijamii, kiuchumi, kimazingira, kisiasa na kidiplomasia.

### 1.4.1 Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo ya akili, utegemezi, moyo, ini na mapafu. Matumizi hayo pia huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini na kifua kikuu miongoni mwa watumiaji na jamii kwa ujumla. Aidha, matumizi hayo yanaweza kufanya mishipa ya damu kusinyaa na inapotokea hali hiyo kwenye ubongo husababisha shinikizo la damu na kiharusi. Matumizi ya kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kuliko alichozoea mtumiaji, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga.

Watumiaji wa dawa za kulevya hasa wanawake wajawazito wamekuwa wakijifungua watoto wenye utegemezi wa dawa za kulevya na mara nyingi wamekuwa na matatizo mengine ya kiafya yakiwemo ya akili na ukuaji wa mtoto. Madhara mengine ya kiafya ni pamoja na saratani, kupoteza mtiririko wa

mawazo na matendo, matatizo ya ini, sonona, kukosa usingizi, kukosa hamu ya kula, kuoza meno, vidonda kwenye mfumo wa chakula, kupunguza nguvu za kiume, magonjwa ya afya ya akili na mara nyingine vifo. Kwa ujumla Matumizi ya dawa za kulevya hupunguza umri wa kuishi na hukatisha maisha ya watumiaji.

### 1.4.2 Kijamii
Dawa za kulevya husababisha mmomonyoko wa maadili, uhalifu, rushwa, unyanyapaa, migogoro ya kifamilia inayosababisha kuvunjika kwa ndoa, watoto wa mitaani na mlundikano kwenye magereza. Pia huzalisha kundi la watu katika jamii ambao wanajiingiza katika biashara ya ngono, kupiga debe na makundi mengine yanayoonekana kutothaminiwa na jamii.

### 1.4.3 Kiusalama
Watumiaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya kihalifu kama vile wizi, ukabaji na uporaji hivyo kusababisha maeneo yenye watumiaji na wauzaji wa dawa za kulevya kuwa na vurugu na kuwa si salama kwa kuishi. Wafanyabiashara wa dawa za kulevya wamekuwa wakifanya vitendo vya kikatili kwa kuwaweka rehani vijana wa kitanzania nje ya nchi ambao hupata mateso makali, ulemavu na wakati mwingine kuuawa pale biashara zisipofanikiwa. Pia matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazoleta ulemavu, vifo na uharibifu wa mali na miundombinu. Aidha fedha inayopatikana kutokana na biashara haramu ya dawa za kulevya inaweza kutumika kufadhili mitandao ya kihalifu.

### 1.4.4 Kiuchumi
Biashara na matumizi ya dawa za kulevya huathiri uchumi wa nchi. Matumizi ya dawa za kulevya hudhoofisha afya za watumiaji ambao kundi kubwa ni vijana hivyo hushindwa kushiriki katika shughuli za uzalishaji kama vile kilimo na viwanda.Vilevile, matumizi ya dawa hizo huathiri sekta ya ajira kwa kuwa watumiaji walio kwenye ajira ufanisi wao hupungua hata wale ambao hawana ajira kutoweza kupata ajira kutokana na kuathiriwa na dawa za kulevya, hali hii hukwamisha ukuaji wa uchumi wa nchi.

Madhara ya kiuchumi yatokanayo na biashara ya dawa za kulevya yameainishwa katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:

**Mfumuko wa bei**
Miongoni mwa madhara ya biashara ya dawa za kulevya ni pamoja na kuwepo kwa mfumuko wa bei ambao husababishwa na wenye fedha nyingi zinazotokana na dawa za kulevya kununua bidhaa kwa bei ya juu hivyo kufanya wananchi wenye kipato cha chini kushindwa kumudu gharama hizo.

**Kuongezeka kwa pengo kati ya walionacho na wasionacho**
Kuongezeka kwa tofauti kati ya wenye nacho na wasio nacho ambapo wenye fedha nyingi zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya huweza kuhodhi sehemu kubwa ya raslimali za jamii kama vile ardhi na kuwaacha wenye kipato cha kawaida bila chochote.

**Kuongezeka kwa ununuzi wa bidhaa toka nje ya nchi na hivyo kuathiri soko la bidhaa za ndani**
Kipato kikubwa kinachotokana na dawa za kuleyva huongeza kasi ya kununua vitu kutoka nje ya nchi hivyo kufanya kudorora kwa uchumi kutokana na kutokuwepo na uwiano sahihi wa bidhaa zinazouzwa nchini na zile zinazoagizwa toka nje ya nchi.

**Kuathirika kwa mizania ya ushindani wa kibiashara**
Ukwasi unaotokana na dawa za kulevya huchochea rushwa ambayo husababisha wafanyabiashara ya dawa za kulevya kuchukua fursa nyingi kama vile za kibiashara hivyo kuwaacha wawekezaji wenye kipato cha kawaida bila fursa.

**Utakatishaji wa fedha haramu**
Biashara ya dawa za kulevya huambatana na utakatishaji wa fedha zinazotokana nabiashara hiyo ambapo madhara yake ni pamoja na kuhama kwa nguvu ya kifedha kutoka kwenye serikali, masoko na wananchi na kwenda kwa wahalifu ambao ni wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Vilevile, utakatishaji fedha huathiri taasisi za kifedha kama vile mabenki pale mhalifu anapoamua kutoa fedha zake kwa mkupuo ambapo mara nyingi huwa ni kiasi kikubwa na hivyo kuiacha taasisi ya kifedha ikiyumba hivyo kuchangia kuzorotesha ukuaji wa uchumi.

### 1.4.5 Kisiasa
Kutokana nauwezo wao mkubwa wa kifedha wafanyabiashara wa dawa za kulevya huweza kujiingiza katika shughuli za kisiasa na hivyo kuwepo na uwezekano wa nchi kupata viongozi wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Pia, wafanyabiashara hao wanaweza kufadhili chaguzi na kuwaweka watu wao madarakani ili kulinda biashara na maslahi yao. Hali hii huweza kuathiri mstakabali wa nchi.

### 1.4.6 Kimazingira
Kilimo cha bangi na mirungi hufanyika katika maeneo yasiyo fikika kirahisi kama vile kwenye milima, misitu na kwenye vyanzo vya maji na hivyo kusababisha madhara makubwa ya kimazingira. Madhara hayo ni pamoja na kukauka kwa vyanzo vya maji, ukame, mmomonyoko wa ardhi na kutoweka kwa

baadhi ya viumbe hai na uoto wa asili. Uharibifu huu umejidhihirisha katika baadhi ya safu za milima ya Uluguru, Usambara, Udzungwa, Uparena maeneo ya Arumeru. Aidha, uchafuzi mkubwa wa mazingira unafanywa na wajidunga ambao wamekuwa wakitupa ovyo mabomba ya sindano katika fukwe, vituo vya daladala, viwanja vya michezo na maeneo mengine mitaani.

# SURA YA PILI

## 2 MWENENDO WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

### 2.1 AFRIKA

Bara la Afrika mwanzo lilikuwa ni sehemu kuu ya kusafirishia dawa za kulevya, lakini kwa sasa hali hii imebadirika na kuwa ni watumiaji na pia soko kuu la jumla la dawa za kulevya.

Uzalishwaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya umeendelea kuwa ni changamoto sehemu kubwa barani Afrika, huku ikikadiriwa kuwepo na ongezeko la matumizi ya bangi kwa asilimia 7.6 kwa mwaka mara mbili ya kiwango cha wastani wa matumizi ya bangi duniani ambacho ni 3.8. Afrika imeendelea kuwa ni eneo linalongoza kwa kilimo na matumizi ya mmea wa bangi ambapo asilimia 14 ya bangi iliyokamatwa duniani ilizalishwa Afrika. Pia kumeripotiwa kuwepo na ongezeko la ukamataji wa bangi iliyosindikwa hasa huko Morocco.

Bangi imeendelea kuwa ni dawa inayotumika zaidi barani Afrika ikifuatiwa na heroin ambayo pia matumizi yake yameongezeka kiasi kikubwa kwa baadhi ya nchi hasa eneo la Afrika Mashariki.Usafirishaji wadawa za kulevya jamii ya afyuni kutoka Afghanistanna maeneo mengine ya Asia, unaongezeka mashariki na magharibi mwa Afrika, ikiwa ni kwa matumizi ya ndani au kusafirishwa kwenda nchi zingine.

Usafirishaji wa dawa za kulevya katika bahari ya Hindi kupitia Afrika Mashariki uliongezeka kwa kasi hasa kwa kufichwa kwenyemakontena ya bidhaa mbalimbali.Aidha, matukio ya kuongezeka kwa mataifa mengi ya Afrika kujihusisha na usafirishaji wa dawa za kulevya yameripotiwa duniani pamoja na kuongezeka kwa mitandao ya magenge ya kihalifu huko Afrika ya Magharibi.

#### a) Ushirikiano wa Kikanda

Kumekuwa na ushirikiano wa kikanda katika jitihada za kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali ya Afrika. Ushirikiano huu ulihusisha operesheni za pamoja, mikutano na mafunzo kwa vyombo vya udhibiti wa dawa za kulevya. Polisi wa Kimataifa (INTERPOL) walifanya operesheni ya kuimarisha mipaka kati yaIvory Coast naNigeria. Operesheni hiyo ilifanikisha ukamatajiwatakribani kilo 900 za dawa za kulevya zikiwemo cocaine, bangi, metamfetamini na mirungi.Vilevile, INCB iliandaa mafunzokwa mamlaka za udhibiti za nchi za Afrika ya Mashariki, mafunzo hayo yalifanyika nchini Kenya mwezi Aprili 2016, ambayo yalihusisha nchi za Burundi, Comoro,

Ethiopia, Kenya, Madagascar, Rwanda, Seychelles, Uganda na Tanzania.

**b) Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji**

**Nakotiki**
Kilimo nausafirishaji wa bangi vimeendelea kuwa ni changamoto kwa Mamlaka za udhibiti wa Dawa za kulevya Afrika. Mwezi Mei mwaka 2016 Mamlaka huko Mali zilikamata kiasi cha Tani 2.7 za bangi ikitokea Ghana. Ukamataji mwingine pia ulifanyika katika nchi za Zambia (tani 17), Madagascar(tani 8), Msumbiji (tani 5), Zimbabwe (tani 1), Ivory Coast (Tani 4),Swaziland (tani 2.2, ekari 70), Mauritius (kilo 43)naMalawi (ekari 37).

Kuna dalili kuwa Afrika hasa Afrika ya Magharibi na Kaskazini zimekuwa zikijihusha kwa kiasi kikubwa na upitishaji wa cocaine kutoka Amerika ya kusini kwenda Ulaya, Amerika ya Kaskazini Asia na sehemu nyingine duniani.Aidha, mwaka 2016 huko Kaskazini mwa Afrika kuripotiwa ukamataji wa cocaine zaidi ya kilo 120 nchini Morocco na kilo 88 za cocaine nchini Algeria.

## 2.2 ULAYA
Biashara ya dawa za kulevya inabaki kuwa moja ya matishio makubwa ya kiusalamakatika nchi za Ulaya. Inakadiriwa moja ya tano ya mapato yanayozalishwa na uhalifu duniani yanatokana na biashara haramu ya dawa za kulevya. Raia wa Umoja wa nchi za Ulaya pekee hutumia kati ya Euro bilioni 21 hadi 31 kila mwaka kwa ajili ya dawa za kulevya.

Bangi hutumiwa zaidi Ulaya na inakadiriwa kwamba watu wazima million 27 wametumia dawa hiyo mwaka mmoja uliopita.mwaka 2014 watumiaji wa cocainebarani Ulaya walikuwa asilimia 0.7 ya watu wenye umri wa miaka 15 – 64 (watu zaidi ya milioni 4). Dawa jamii ya afyuni inayotumiwa Ulaya ni ile inayozalishwa zaidi. Afghanistan na kusafirishwa Ulaya kwa kutumia njia kuu mbili za Balkan ya Kaskazini. Amfetamini au metamfetamini zimekadiriwa kutumiwa na watu wanaokadiriwa kuwa Milioni 2.4 barani Ulaya kwa kipidi cha mwaka uliopita. Katika nchi za Jamuiya ya Ulaya, matumizi ya vichangamshi (Synthetic stimulants) ambazo ni amfetamini, metamfetamini na MDMA pamoja ni makubwa kidogo zaidi ya yale ya cocaine.Jumuiya ya Ulaya iligundua zaidi ya dawa mpya za kulevya 560, ikilinganishwa naaina 100 ziliripotiwa mwaka 2015.

## 2.3 ASIA
### 2.3.1 Mashariki na Kusini – mashariki mwa Asia
Uzalishaji wa dawa za kulevya jamii ya Afyuni pamoja na usafirishaji wake unaendelea kuleta shaka kwa kuwa kilimo cha afyuni kiliendelea kuongezeka.

Mwaka 2015, eneo lote lililolimwa afyuni lilibaki kuwa juu Ndrini Myanmar kwa mwaka wa tatu mfululizo likikadiriwa kuwa hekta 55,500 huku Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Lao kilimo kikipungua lakini sio sana. Usafirishaji wa afyuni na Kemikali bashirifu kati ya China na Myanmar uliendelea ukichagizwa na faida na soko kubwa vilivyopo katika eneo hilo. Lipo pia tatizo la utengenezaji na usafirishaji wa ATS hasa metamfetamini ambayo imekuwa ikikamatwa kwa wingi hali inayohitaji ushirikiano katika kulinda mipaka ya nchi zilizopo eneo hilo. Soko la dawa mpya za kulevya linaendelea kupanda na kuleta mashaka ya kiafya kwenye eneo hilo, kwani Sheria zilizopo katika nchi nyingi za eneo hilo hazifai kukabiliana na kukua na kuibuka kwa dawa hizo.

### a) Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

**Nakotiki**

Kilimo cha afyuni kiliendelea kufanyika katika nchi za Laosna Myanmar. Nchi hizi zilikadiriwa kuzalisha tani 800 za afyuni mwaka 2015 na kuwa wasambazaji wakuu katika eneo la Oceania na Asia Magharibi. Nchi ya Myanmar inabaki kuwa ya pili duniani kwa kilimo cha afyuni. Ukamataji wa heroin na Morphine Mashariki na Kusini Mashariki mwa Asia uliongezeka mara mbili kati ya miaka ya 2008 na 2014 kutoka tani 5.7 hadi tani 13. China imeendelea kuwa ni soko kubwa la heroin na mzalishaji wa kemikali bashirifu inayosafirishwa kimagendo kwenda nchi jirani.

Kilimo cha bangi kwenye baadhi ya nchi za eneo hilo kiliendelea na kuripotiwa katika nchi za Indonesia, Philippines, Myanmar na Vietnam. Mwaka 2015 kiasi cha tani 29 cha bangi kilikamatwa nchini Indonesia, wakati China ilikamata tani 8.7.

**Saikotropiki**

Kumekuwa na ongezeko la usafirishaji wa ATS mwaka 2015 kwa asilimia 35 kulinganisha na mwaka 2014, ambapo tani 36.6 za metamfetamini zilikamatwa nchini China. Nchi nyingine zilizokamata metamfetamini ni pamoja na Mynmar na Indonesia. Nchi za Afrika zikiwemo Ghana, Kenya, Mali na Afika Kusini zimetambuliwa kuwa chanzo cha Metamfetamini inayoingizwa nchini Jamhuri ya Korea. Kiasi kikubwa cha utengenezaji na usafirishaji wa metamfetamini ya mawe (Crystalline) inaendelea kuwa tishio zaidi katika nchi za eneo hilo. China iliharibu maabara nyingi haramu zinazotengeneza metamfetamini ya mawe mwaka 2015 na karibu kesi 500 za utengenezaji haramu ziligunduliwa nchini humo. Mynmar pia ilihusika katika utengenezaji wa metamfetamini ya mawe.

Mwaka 2014 UNODC ilikadiria kuwa jumla ya vidonge vinavyokadiriwa milioni 244 vya metamfetamini vilikamatwa katika eneo hilo. Ukamataji mkubwa kwa mkupuo mmoja na vidonge milioni 26.7 uliripotiwa Myanmar Julai, 2015. Eneo hilo limeripoti ongezeko la idadi ya dawampya za kulevya mbadala wa "ecstacy" katika miaka ya karibuni hasa kutokana na udhibiti mkali wa kemikali bashirifu. Katika eneo lote kumeripotiwa ukamataji wa "ecstacy" isiyo na MDMA lakini hasa na kemikali zisizodhibitiwa kisheria.

**Kemikali Bashirifu**

Kilimo cha mimea ya afyuni na mahitaji ya ATS vikiendelea kupanda, utengenezaji na usafirishaji wa kemikali bashirifu katika eneo hili unaendelea. Kemikali zinazotumiwa kutengeneza heroin (acetic anhydride) na ATS (ephedrine na pseudoephedrine) zimekuwa zikisafirishwa kutoka China na India kwenda nchi mbalimbali kwenye eneo hili. Mwaka 2014, Cambodia ilikamata kiasi kikubwa cha "ephedrine" na kemikali nyingine bashirifu, wakati mwaka 2015, China nayo ilikamata karibu tani 1,600 za kemikali bashirifu.

Uwepo wa viwanda vya utengenezaji kemikali zenye matumizi halali katika eneo hili kumechangia hatari ya kuchepushwa kwa kemikali hizo kutoka vyanzo halali kama ilivyoripotiwa nchini China katika miaka ya karibuni. Changamoto kubwa inaletwa nadawa mpya zinazotengenezwa kutopkana na kemikali bashirifu ambazo hazipo kwenye orodha ya jedwali la udhibiti kimataifa yaani 2-bromo propiophenone, ambayo ni mbadala wa ephedrine na mmea wa "Ephedra".

**Dawa za kulevya na kemikali bashirifu zisizodhibitiwa kimataifa**

Kiasi cha "Ketamine" kilichokamatwa katika eneo hili kiliongezeka kutoka tani 6 mwaka 2012 hadi, tani 12 mwaka 2014. Nchini China kiasi cha "Ketamine iliyokamatwa kilipanda zaidi ya mara nne kutoka tani 4.7 mwaka 2012 hadi tani 19.6 mwaka 2015. China ni nchi inayoongoza kwa kuharibu maabara haramu zinazotengeneza "ketamine" ambapo inakadiriwa maabara 100 huharibiwa kwa mwaka. Vilevile, Agosti, 2016 Malaysia iliharibu maabara haramu ya kwanza inayotengeneza "ketamine"na kilo 269 za ketamine ya mawe na ya kimiminika ilikamatwa.

Dawa mpya za kulevya zimeendelea kutengenezwa na kusafirishwa katika eneo hili. Kwa mfano, nchini Singapore dawa mpya zilizokamatwa ziliongezeka kutoka vidonge 470 mwaka 2014 hadi vidonge 3,000 mwaka 2015. China, iliorodhesha aina 116 za dawa mpya zikiwemo "Cannabinoids", cathinones, phenylethylamines na piperazines zinazozalishwa nchini humo.

Eneo hili pia limeendelea kuripoti usafirishaji na uwepo wa mimea yenye kulevya jamii ya mirungi (Catha edulis) na "Kratom" (Mitragyna speciosa) ambapo mimea jamii ya mirungi ikitokea Afrika Mashariki na Rasi ya Arabuni. Tani 4.4 za Mirungi zilizokamatwa kwa vipindi viwili ziliripotiwa na nchi ya Vietnam katikati ya mwaka 2016.

### 2.3.2 Asia Kusini

Mwaka 2015, liliendelea kukumbwa na usafirishaji wa dawa jamii ya afyuni, bangi na dawa mpya za kulevya, utengenezaji na usafirishaji wa metamfetamini, uchepushwaji wa dawa tiba zenye madhara ya kulevya. Mwaka 2015, Bhutan ilianza kutoa matibabu kwa watumiaji wa dawa jamii ya afyuni kwa kutumia buprenorphine.

**Kilimo, uzalishaji, utengenezaji na usafirishaji**

**Nakotiki**

Mwaka 2015 nchini India kilimo cha mimea ya bangi kilikuwa zaidi ya hekta 313 hata hivyo idadi ya matukio ya ukamataji wa bangi iliongezeka, ingawa jumla ya kiwango kilicho kamatwa kilipungua. Aidha, India inazalisha bangi ya kusindika na kiasi kingine huingizwa kutoka Nepal, ambapo asilimia 21.9 ya bangi yakusindikwa iliyokamatwa nchini India mwaka 2015 ilitokea Nepal. Kiasi cha ukamataji wa bangi nchini Bangladesh kiliongezeka kutoka tani 35 mwaka 2014 hadi tani 41 mwaka 2015. Nchi nyingine zinazolima bangi ni Bhutan na Sri Lanka. Kiwango cha morphine kilichokamatwa nchini India kiliongezeka kutoka kilo 25 mwaka 2014 hadi kilo 61 mwaka 2015. Ukamataji wa heroin pia uliongezeka kidogo kwa mwaka huo, Kiwango cha heroin kilichokamatwa Sri Lanka mwaka 2016, kiliongezeka hadi kilo 134 ukilinganisha na kilo 18 zilizokamatwa mwaka 2015.

**Saikotropiki**

India ilikamata jumla ya kilo 166 za ATS mwaka 2015 chini kidogo ya kilo 196 zilizokamatwa mwaka 2014 na vilevile iliharibu duka moja haramu la dawa la Intaneti (illicit Internet pharmacy) na kukamata vidonge 14,310 vyenye nakotiki na uzito wa kilo 227 kwa mwaka 2015. Ukamataji wa mandrax (methaqualone) uliongezeka nchini India kutoka kilo 54 mwaka 2014 kufikia kilo 89 mwaka 2015. Usafirishaji wa "yaba" (Metamfetamini ya vidonge) kutoka Myanmar kwenda Bangladesh uliongezeka ambapo Januari, 2016, vidonge milioni 2.8 vilikamatwa ukiwa ni ukamataji mkubwa zaidi kufanyika nchini humo.

**Kemikali Bashirifu**

India inakabiliwa na changamoto ya udhibiti wa uchepushwaji wa ephedrine na Pseudoephedrine. Mwaka 2015, kiasi kikubwa cha vidonge vyenye

pseudoephedrine au ephedrine vilikamatwa mpakani mwa India na Myanmar kukiwa na uwezekano wa kuingizwa nchini Myanmar ili kutengeneza ATS.

**Dawa zisizodhibitiwa Kimataifa**

Kumekuwa na ongezeko la ukamataji wa Ketamine inayosafirishwa kutoka India kwenda Kusini-Mashariki mwa Asia, ambapo kilo 2011.6 zilikamatwa mwaka 2015 ikilinganishwa na kilo 20.4 zilizokamatwa mwaka 2014. Hii ilidhihirisha kuwaIndia inaendelea kuwa chanzo cha Ketamine katika eneo hilo.Pia kumekuwa na, matukio ya kutumia huduma za usafirishaji wa vifurushi kusafirisha Ketamine kwenda Afrika Kusini na Uingereza.Dawa mpya za kulevya zinazotambuliwa kutokea eneo hili, zimesababisha INCB kuhimiza Serikali za eneo hili kushirikiana katika kudhibiti dawa hizo mpya.

### 2.3.3 Asia Magharibi

Kilimo cha mimea ya afyuni nchini Afhanistan, ndio tatizo kubwa kwenye eneo hili pamoja na maeneo mengine duniani.Juhudi za kudhibiti tatizo hili zinakwamishwa na rushwa, Ugaidi na vita katika nchi za Iraq, Syria na Yemen huku kukiwa na wimbi kubwa la wakimbizi kwenye makambi yaliyopo nchi za Jordan, Lebanon na Uturuki.

**a) Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirshaji**

**Nakotiki**

Afghanistan inaendelea kuwa chanzo kikuu cha uzalishaji wa dawa jamii ya afyuni katika eneo hili ambalo pia limekuwa na ukamataji mkubwa. Miongoni mwa njia kuu tatu za usafirishaji maarufu zaidi ni ile ya Balkan inayoptia Iran na Uturuki kufikia masoko yaliyopo Ulaya. Hata hivyo, zipo njia nyingine zemeanza kupata umaarufu ambapo Uturuki imeripoti kuibuka taratibu kwa njia nyingine ya Balkan inayojumuisha Iraq na Syria ikiwa ni nyongeza ya ile ya asili.

Kumekuwa na ongezeko la eneo lianaloliama Afyuni kwa asilimaia 10 nchini Afganisatan kulinganisha na mwaka 2015 likifikia hekta 201,000 mwaka 2016. Jimbo la Helmand lilibakia kuwa mzalishaji mkuu kwa mwaka 2016. Lebanon na Uzbekistan nazo ziliripoti kuwepo kwa mimea ya afyuni katika nchi zao.

Nchi za Afghanistan, Lebanon na Pakistan ndizo zinazozalisha zaidi bangi ya kusindik katika eneo hili. Mwaka 2015 Saudi Arabia ilikamata kiasi kikubwa cha bangi kikikaribia tani 3.Ukamataji wacocaine eneo hili ni mdogo, ingawa ulipanda mara tatu katika kipindi cha miaka kumi iliyopita na asilimia 50 ya ukamataji huo ukifanyika eneo la Mashariki ya Kati. Israel inatajwa mara nyingi kuwa ni eneo la mwisho linalopokea cocaini inayotoka Latin Amerika kuingizwa

katika eneo hili.

**Saikotropiki**

Nchi za eneo hili hasa Mashariki ya Kati na eneo la Ghuba zinaendelea kuzalisha, kupitisha na kupokea metamfetamini na amfetamini. Piavidonge jamii ya amfetamini(captagon) vimekamatwa kwa wingi kwenye eneo hilo. Lebanon na Uturuki kila moja zilikamata zaidi ya vidonge Milioni 15 mwaka 2015, Jordan pia ilikamata vidonge Milioni 13 mwaka 2016.

**Kemikali Bashirifu**

Eneo hili lilikabiliwa na uzalishaji wa dawa za kulevya kwa kutumia kemikali bashirifu zinazochepushwa ambazo ni acetic anhydride inayotumika kutengeneza heroin, ephedrine, pseudoephedrine, phenyl propanone, Phenylacetic acid zinayotumika kutengeneza ATS na kemikali nyingine.

"Acetic anhydride" huingizwa nchini Afghanistan kutoka Iran na Pakistani ambapo kiasi kikubwa kimeendelea kukamatwa katika miaka ya 2015 na 2016. Usafirishaji wa kemikali hii umeendelea kupungua nchini Afghanistan kutokana na wachepushaji kutumia kemikali zisizoorodheshwa au kudhibitiwa kisheria. Mamlaka za Afghanistan zimegundua ongezeko la kemikali bashirifu zinazotengeneza metamfetamini nchini humo.

## 2.4 AMERIKA

Bara la Amerika liliendelea kukumbwa tatizo la dawa za kulevya ikiwemo matumizi ya dawa hizo, kuibuka kwa kemikali za kutengeneza dawa za kulevya, kilimo cha mimea ya koka na afyuni, utengenezaji wa dawa za kulevya na uchepushwaji wa kemikali bashirifu.

### 2.4.1 Amerika ya Kati na Caribbean

Amerika ya Kati na Carribean zimeendelea kupitisha cocaine kutoka nchi zalishaji hasa Colombia kwenda nchini Marekani kwenye soko kubwa la dawa hizi ikifuatiwa na Canada na Ulaya. Aidha, kulikuwepo na ushirikiano katika ya UNODC na nchi zilizopo kwenye ukanda huu katika kupambana na magenge ya kihalifu na biashara ya dawa za kulevya. Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yameimarishwa kwakuandaa Sera, Sheria pamoja na vyombo vya kudhibiti biashara na matumizi ya dawa hizi.

**a) Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji wa dawa za kulevya Nakotiki**

Panama ambayo inaongoza kwa ukamataji wa cocaine katika eneo hili iliongezeka ukamataji kwa asilimia 32 mwaka 2015 ikilinganishwa na wa mwaka

2014. Ongezeko hili la ukamataji kuhusishwa na ongezeko kilimo cha coca nchini Colombia kwa mwaka huo.

bangi iliyokamatwa mwaka 2014 Carribean ni asilimia 13 ya bangi iliyokamatwa duniani kote. Kiasi cha ukamati wa bangi katika eneo hilo kimekuwa kikiongezeka ambapo Jamaica ilikuwa chanzo kikuu cha mfumo haramu wa kimataifa wa usafirishaji wa bangi. Inakadiriwa kuwa mwaka 2015 kulikuwa na kiasi cha hekta15000 za mashamba ya bangi nchini Jamaica ambapo kiasi cha hekta 725 za mashamba hayo ziliteketezwa.

Guatemala ni nchi pekee katika eneo hili inayozalisha afyuni ingawa ukamataji wa heroin nchini Guatemala ulipungua kutoka kilo 134 mwaka 2014 hadi kilo 83 mwaka 2015. Upungufu huo ulienda sambamba na kuongezeka kwa uzalishaji wa opium nchini Mexico na kuharibiwa kwa mitandao mikubwa ya usafirishaji wa dawa za kulevya nchini Guatemala na kupungua kwa kasi kwa bei ya afyuni kwa asilimia 77 kulikosababisha wakulima kuacha kulima zao hilo na kujishughulisha na kilimo cha mahindi, nyanya na mazao mengine halali mwaka 2015.

**Saikotropiki**

Guatemala ni nchi pekee katika eneo la Amerika ya Kati na Carribean iliyoharibu maabara haramu zilizokuwa zinatumika kutengeneza amphetamine katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Mwaka 2013 ziliharibiwa maabara 8 na mwaka 2014 maabara 9 ambapo nne kati ya hizo zilikuwa zinatumika kutengeneza amphetamine na tano methamphetamine.Wakati nchi hii ilikuwa imeathirika kwa kiasi kidogo kwa utengenezaji na usafirishaji wa ATS, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita baadhi ya nchi mara kwa mara zimetoa taarifa ya kukamata kwa dawa za kulevya aina ya ecstasy na lysergic aciddiethylamide (LSD)

**Kemikali Bashirifu**

Utengenezaji wa ATS uliendelea kuwa changamoto nchini Guatemala kutokana na ukamataji wa kemikali bashirifu katika eneo hilo ambapo, mwaka 2015 zilikamatwa tani 25 za kemikali bashirifu katika bandari za nchi hiyo.

### 2.4.2 Amerika ya Kaskazini

Mwaka 2016 Pennsylavia lilikuwa jimbo la 24 nchini Marekani kutunga sheria ya kuruhusu matumizi ya bangi kwa ajili ya tiba ikifuatiwa na Ohio. Pia, majimbo ya Arkansas, Florida na Dakota Kaskazini yalipiga kura ya kuruhusu bangi kutumika kwa ajili ya matumizi ya tiba. Aidha majimbo ya Califonia, Maine, Massachusetts na Nevada walipitisha maamuzi ya kuweza kuhalalisha na kuweka vigezo vya matumizi ya bangi.

Tatizo la matumizi ya dawa za tiba jamii ya Opioid na heroin liliendelea kuikumba Marekani. Mwaka 2015 watumiaji zaidi ya 47,000 wa dawa hizo walifariki kutokana na kuzidisha kiwango cha matumizi, kati yao18,000vifo vyao vilitokana matumizi ya dawa za kutuliza maumivu jamii ya opioid na vifo vya zaidi ya watu 10,000 vilitokana na matumizi ya heroin.

### a) Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji wa dawa za kulevya

**Nakotiki**

Kutokana na taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2016, mwaka 2009 hadi 2014 Marekani ilifanikiwa kukamata jumla ya asilimia 15 ya cocaine iliyokuwepo dunia nzima. Ukamataji huo uliifanya Marekani kushika nafasi ya pili duniani ikitanguliwa na Colombia. Nchi ya Marekani ilikuwa ya kwanza kwa ukamataji wa cocaine katika Bara la Amerika ya Kaskazini kwa kipindi cha kuanzia miaka ya 2009 hadi 2014 kwa asilimia 95 ya cocaine iliyokamatwa katika bara hilo ikifuatiwa na Mexico ambayo ilifanikiwa kukamata asilimia 8 tu.

Heroin iliyoingia Canada ilitokea Afghanistan na iliyoingia nchini Marekani ilitokea Columbia na Mexico. Mwaka 2016 Marekani ilikamata kiasi kikubwa cha heroin ambacho kilikuwa ni ongezeko la asilimia 80 ya ukamataji wa heroin iliyowahi kukamatwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kutoka zaidi ya tani 3.7 mwaka 2011 hadi tani 6.8 mwaka 2015. Ukamataji huu uliashiria kuongezeka kwa upatikanaji wa heroin nchini humo ulioenda sambamba na ongezeko la matumizi ya heroin pamoja na vifo vilivyotokana na matumizi yake ambavyo viliongezeka kutoka 3,036 mwaka 2010 hadi kufikia 10,574 mwaka 2014.

Nchini Mexico uteketezaji wa mashamba ya afyuni uliongezeka kutoka hekari 21,000mwaka 2014 kufikia hekari 26,000 Mwaka 2015.Mwaka 2016, Serikali ya Canada ilipiga marufuku kilimo cha afyuni isipokuwa kwa matumizi ya kisayansi.

Bangi iliendelea kuwa dawa ya kulevya iliyolimwa, kuzalishwa, kusafirishwa na kutumiwa kwa wingi kuliko dawa nyingine ya kulevya katika Bara la Amerika ya Kaskazini na duniani kwa ujumla. Mwaka 2015 nchi ya Marekani ilifanikiwa kuteketeza kiasi cha miche milioni 4 (cultivated outdoor) na zaidi ya miche 320,000 (indoor plants). Pia, mali zilizotaifishwa kutokana na biashara ya bangi zilikadiriwa kuwa na thamani ya dola za kimarekani milioni 30.

**Kemikali Bashirifu**

Mwaka 2015 kulikuwa na ongezeko la kiasi cha asilimia 38 cha uteketezaji wa maabara haramu nchini Mexico. Imegundulika kuwa tofauti na miaka ya nyuma ambapo kemikali bashirifu aina ya esters na phynylacetic acid zilikuwa

zikitumika kutengenezea metahamphetamine kumekuwa na njia mpyaya kutumia kemikali bashirifu aina ya benzaldehyde na nitroethane.

**Dawa zisizodhibitiwa Kimataifa**

Dawa mpya za kulevya zisizodhibitiwa kimataifa ziemeendelea kuikumba nchi ya Marekani.uwepo wa bangi ya ianyotengenezwa kiwandani na maabara haramu ziliongezeka kutoka maabara 23 mwaka 2009 hadi 37,500 mwaka 2014.Vilevile, cathinones za kutengenezwa ziliongezeka kutoka 29 mwaka 2009 hadi 14,070 mwaka 2014.Bangi ya kutengeneza imeendelea kutawala soko la dawa mpya za kulevya duniani ambapo jumla ya tani 32 za bangi hiyo zilikamatwa.Aidha, ukamataji wa mirungi ulipungua nchini humo. Katika kipindi cha kati ya mwezi Februari 2014 hadi Julai 2016, zaidi ya tani 55 za kratom zilikamatwa na vyombo vya dola nchini marekani.

### 2.4.3 Amerika ya Kusini

Eneo la Amerika Kusini likiendelea kukumbwa na tatizo la uzalishaji wa dawa za kulevya na usafirishaji wa dawa hizo kutokana na uwepo wa mipaka yenye vipenyo vingi, makosa ya kijinai, rushwa na ubovu wa mfumo wa utoaji haki

Aidha, jitihada mbalimbali za kudhibiti dawa za kulevya eneo la Amerika Kusini ziliendelea kufanyika zikiwemo; mafunzo mbalimbali yanayohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya, mikutano ya kuangalia namna ya kuanzisha shughuli za maendeleo mbadala pamoja na kutunga sera na sheria mbalimbali za kudhibiti dawa za kulevya.

**Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji wa dawa za kulevya**

**Nakotiki**

Kuongezeka kwa ukamataji wa bangi katika eneo la Amerika Kusini kuliashiria kuwepo kwa kilimo na uzalishaji, matumizi pamoja na usafirishaji wa bangi katika eneo hilo. Mwaka 2014 kulikuwana ukamataji wa bangi kiasi cha tani 1,457 nchini Uruguay. Paraguay tani 510, Colombia tani 247, Argentina tani 206 na Venezuela tani 26. Ukubwa wa eneo la mashamba ya bangi nchini Columbia lilikuwa ekari 2,783 ambapo kila ekariilikadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha kilo 3000 za bangi. Mwaka 2015 Serikali ya Paraguay ilifanikiwa kuteketeza miche milioni 12.1 ya bangi.

Eneo la Amerika ya Kusini lilibaki kuwa msambazaji mkubwa wa cocaine duniani kwa ajili matumizi. Aidha, eneo hili liiliendelea kuongoza duniani katika ukamataji wa kiasi kikubwa cha cocaine. eneo kwa ajili ya kilimo cha koka nchini Columbia liliongezeka kwaasilimia 39 na mara mbili ya ukubwa wa eneo

lililolimwa koka kwa mwaka 2013. Aidha, ripoti hii ilieleza kuwa picha zilizopigwa kwa kutumia 'satellite' zilionyesha mashamba makubwa ya koka kwenye mbuga za wanyama katika nchi zinazolima koka za Bolivia, Colombia na Peru.

Program za maendeleo mbadala nchini Columbia na Peru zimesaidia kudhoofisha makundi ya kihalifu na magenge ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Mwaka 2015 ukubwa wa eneo lililotumika kupanda mimea ya kokaulipungua nchini Peru na kufikia ekari40,300 ambalo lilikuwa eneo dogo kwa asilimia 6 ukilinganisha na eneo la ekari 42,900 kwa mwaka 2014. Hii ilidhihirisha kupungua kwa kilimo cha koka ambacho kwa miaka ya nyuma kilikuwa katika kiwango cha juu mfano mwaka 2011 kilifikia ekari 62500.

Afyuni hulimwa kwa kiasi kidogo ukilinganisha na bangi pamoja na koka katika eneo la Amerika ya Kusini. Mwaka 2015 kulikuwa na ukamataji wa kiasi cha kilo 393 za heroin nakilo 25 za morphine. Ukamataji huu ulidhihirisha kuongezeka ukamataji wa heroin na kupungua ukamataji wa morphine ukilinganisha na miaka iliyopita.

Columbia inaongoza kwa utengenezaji wa cocaine ikifuatiwa na Peru na Bolvia. Hatahivyo, maabara haramu ziligundulika katika nchi nyingine za Argentina, Brazil, Chile na Ecuador. Mwaka 2015 maabara haramu zipatazo 73 za kutengeneza cocaine nchini Bolvia na maabara zipatazo 3,850 nchini Columbia ziliharibiwa

**Saikotropiki**
Ukamataji wa amfetamini ulifanyika nchini Colombia, Paraguay na Uruguay mwaka 2015 ambapo Columbia ilikamata kiasi cha uniti 121 za ecstasy.

**Dawa zisizodhibitiwa Kimataifa**
Dawa mpya za kulevya zimeendelea kuwa tatizo katika nchi za Argentina, Brazil, Chile, Columbia, Ecuador na Uruguay. Aina ya dawa hizo ni phenethylamines, bangi pamoja na mirungi ya kutengeneza, piperazines na dawa za kulevya za mimea.

## 2.5 OCEANIA
Eneo la Oceania limetawaliwa na methamphetamine hasa nchi za Australia na New Zealand. Ukamataji wa methamphetamine katika nchi nyingine zilizo katika eneo la Oceania kama vile Fiji inaonesha kuwa eneo hili lilitumika kama njia ya kupitisha dawa za kulevya zinazotumika ndani ya eneo hili na zinazosafirishwa kwenda maeneo mengine.

Ushirikianao wa kikanda umeimarishwa ambapo vyombo vya dola vya kikanda vimeundwa na mikutano mbalimbali imefanyika kwa lengo la kubadilishana taarifa za kiintelijensia ili kuimarisha usalama mipakani dhidi ya uhalifu unaovuka mipaka na uhalifu wa kutumia mitandao

Oceaniani eneo pekee duniani ambalo halifuati masharti na matakwa ya Mikataba ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya. Mfano, Nchi za Kiribati na Tuvalu hazijawahi kuendana na matakwa ya mikataba yote mitatu ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya. Kisiwa cha Cook, Nauru, Niue, Samoa na Vanuatu sio wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kudhibiti Dawa za Kulevya wa Mwaka 1961 au wa Mwaka 1971. Nchi ya Solomoni sio mwanachama wa Mkataba wa Mwaka 1988.

**a) Kilimo, Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji wa dawa za kulevya**

**Nakotiki**

Bangi iliendeleakuwani tatizo katika eneo la Oceania. Kiasi cha bangi kilichokamatwa nchini Australia kilikuwa ni kikubwa katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015 ambacho kilifika tani 6. Aidha, kiasi hicho ni pungufu ikilinganishwa na kiasi cha tani zaidi ya 7 kwa mwaka 2013 hadi 2014.Vilevile, Bangi iliyokamatwa nchini New Zealand iliongezeka kutoka kilo 518 kwa mwaka 2014 hadi kilo 692 mwaka 2015. New Zealand wakati wa msimu wa kilimo cha bangi mwaka 2015 hadi 2016 ilifanikisha ukamataji wa zaidi ya miche 130,000 na kilo 80 za bangi kiasi ambacho ni cha pili kwa ukubwa kuwahi kukamatwa katika kipindi cha miaka tisa iliyopita.

Kiasi cha heroin kilichokamatwa katika eneo hili kiliongezeka kwa asilimia 168 kutoka kilo 118.9 kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014 hadi kilo 318.7 kwa kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015. Pia, kiasi cha heroin kilichokamatwa nchini Australia kiliongezeka kutoka kilo 158 kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014 hadi kilo 477 katika kipindi cha mwaka 2014 hado 2015. Kiasi hicho ni cha pili kwa ukubwa kuwahi kukamatwa katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita.

Cocaine iliyokamatwa nchini Australia ni sawa na asilimia 99 ya cocaine iliyokamatwa eneo la Oceania kati ya mwaka 1988 na 2014. Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa mipakani kiliongezeka kutoka kilo 245.6 kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014 kwenda kilo 514.4 katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015. Hatahivyo, kiasi hiki ni nusu tu ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2012-2013.

Kufuatia kupungua kwa kiasi cha cocaine kilichokamatwa nchini New Zealand kutoka kilo 10.2 mwaka 2014 hadi gramu 129 mwaka 2015, kiasi kikubwa cha

cocaine kilo 35 kilikamatwa nchini humo mwezi Mei 2016 kikitokea Mexico. Ukamataji mwingine wa kiasi kikubwa cha cocaine eneo la Pacific ulihusisha kilo 50 nchini Fiji mwaka 2015 na ule wa kilo 680 kwenye mtumbwi eneo la French Polynesia mwezi Februari 2016. Hali hii inadhihirisha uwepo wa njia mbalimbali za usafirishaji ndani ya eneo la Oceania kwenda nchi za Australia na New Zealand.

**Saikotropiki**

katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015, Austaralia ilikamata tani 12.6 za ATS kiasi ambacho ni kikubwa zaidi ya mara tatu kutoka tani 4.1 kilichokamatwa mwaka 2013 hadi 2014. Kiasi cha ATS ukiondoa ecstasy kilichokamatwa kwenye mpaka wa Australia kiliongezeka mara mbili kutoka tani 1.8 mwaka 2013 hadi 2014 hadi tani 3.4 mwaka 2014 hadi 2015. Ukamataji wa methamphetamine ya mawe ulikuwa asilimia 76.4 ya uzito wa ATS iliyokamatwa mipakani katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015.

Kiasi cha methamphetamine kilichokamatwa nchini New Zealand kilikuwa ni zaidi ya mara tatu kutoka kilo 98.8 mwaka 2014 na kilo 334.3 mwaka 2015. Hatahivyo, kiasi cha kilo 79.3 za methamphetamine zilizokamatwa na maafisa forodha kilihisiwa kuwa kilikuwa kinaelekea Australia. Mwezi Juni 2016 kilikamatwa kiasi cha kilo 494 za methamphetamine nchini Australia ambazo zilitengenezwa nchini New Zealand.

Ecstasy iliyokamatwa katika mipaka ya Australia iliongezeka kwa tani 2 katika kipindi cha 2014 hadi 2015, ikiwa ni kiasi kikubwa ambacho ni mara ya pili kuwahi kukamatwa kwa miongo miwili iliyopita, ikilinganishwa na kilo 94. 8 zilizokamatwa katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014. Ukamataji wa mara moja wa ecstacy wa kiasi cha tani 1.9 zilizokuwa zimefichwa kwenye mizigo iliyokuwa inasafirishwa kwa njia ya bahari ulikuwa ni asilimia 95.8 zilizokamatwa kwenye mipaka katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015.

**Kemikali Bashirifu**

Kiasi kikubwa cha methamphetamine zilizokamatwa nchini Australia, zilitengenezwa kutokana na ephedrine na pseudoephedrine. Kiasi cha ATS zisizo na ecstasy zilizokamatwa katika mipaka ya Australia kilipungua kutoka tani 1.5 kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014 na kufikia tani 0.5 katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015. Ukamataji wa kiasi kikubwa cha ephedrine wa jumla ya kilo 340 ulifanyika nchini Austaralia mwezi Januari 2016. Ukamataji huu ni tofauti na ukamataji wa kemikali bashirifu za ecstasy uliofanyika mipakani ambao uliongezeka kutoka kilo 1.24 kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014 hadi kilo 288 mwaka 2014 hadi 2015.

Maabara haramu ndogo ziligunduliwa katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015 ziliongezeka nakufikia asilimia 60.9. Kiasi kikubwa cha maabara ndogo zilitumika kutengeneza amphetamine na maabara za kutengeza ecstasy ziliongezeka kutoka maabara 3 mwaka 2013 hadi 2014 na kufikia maabara 18 mwaka 2014 hadi 2015.

Matumizi ya ephedrine kwa ajili ya kutengeneza methamphetamine yaliendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa nchini New Zealand mwaka 2015 hadi 2016. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 92 ya kilo 966.6 za kemikali ya hiyo iliyokamatwa mwaka 2015. Kiasi cha kilo 95 za ephedrine zilikamatwa nchini New Zealand mwezi Oktoba 2015 na kilo 200 zilikamatwa mwezi Aprili 2016. Kiasi cha maabara haramu zilizoharibiwa nchini News Zealand kilipungua kutoka 82 mwaka 2014 hadi 69 mwaka 2015.

**Dawa zisizodhibitiwa Kimataifa**

Dawa mpya za kulevya ziliendelea kukugunduliwa katika mpaka wa Australia ambapo kulikuwa na matukio 551 ya ukamataji mwaka 2014 hadi 2015 na matukio 92 ya ukamataji mwaka 2013 hadi 2015. Hata hivyo, kiasi cha dawa hizo kilipungua kutoka kilo 543 kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014 na kufikia kilo 52.7 katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015, ikiwa ni mara ya pili kukamata kiasi kidogo. Kiasi kikubwa cha dawa mpya za kulevya zenye cathinone ambazo zilifanyiwa uchunguzi zilikuwa ni asilimia 71.1 zikifuatiwa na zile zenye synthetic cannabinoids kwa asilimia 22.8. Kugunduliwa kwa ketamine kwenye mipaka ya Australia kuliongezeka kutoka 155 mwaka 2013 hadi 2014 na kufikia 218 katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015. Vilevile, usafirishaji wa dawa hizi kimataifa kwa njia ya vifurushi ulifikia asilimia 97.2.

# SURA YA TATU

## 3 UDHIBITI NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanaongozwa na nguzo kuu tatu ambazo ni udhibiti wa upatikana wa dawa za kulevya, udhibiti wa utumiaji wa dawaza kulevya na kupunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya.

### 3.1 Mapambano Dhidi ya Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Mwaka 2016 Serikali iliimarisha udhibiti wa dawa za kulevya katika mipaka ya Tunduma, Kasumulo, Namanga na Horohoro, kwa kutoa, Elimu kwa watendaji juu ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 pamoja na matumizi ya vifaa vya utambuzi wa dawa za kulevya.

Mwaka 2016 Serikali ilikamilisha rasimu ya kwanza ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 baada ya kuonekana na changamoto za kiutekelezaji kama; kutoharamisha kwa baadhi ya vitendo vya kihalifu vikiwemo vya wafanyabiashara wa dawa za kulevya kuweka watu rehani nje ya nchi ili kufanikisha biashara yao.Vilevile, Serikali ilipiga marufuku matumizi ya tumbaku ijulikanayo kama Shisha ambayo kwa utafiti mdogo uliofanyika nchini ulionyesha kuwa baadhi ya watumiaji wakiwemo wanafunzi walikuwa wanaitumia kwa kuchanganya au kuchanganyiwa na dawa za kulevya. Aidha, tumbaku iliyokuwa ikitumika kwenye shisha ilidhihirika kuwa na kiwango kikubwa cha kemikali aina ya nikotini ambayo ina madhara makubwa kiafya.

#### 3.1.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu

Serikali kupitia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali husimamia na kudhibiti kemikali bashirifu chini ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Na. 3 ya Mwaka 2003. Kemikali bashirifu zinazosimamiwa na kudhibitiwa na sheria hii ni pamoja na; Acetic anhydride, Acetone, Ethyl ether, Hydrochloric acid, 3,4-Methylene-dioxy-phenyl-2-propanone, Methyl ethyl ketone, 1-Phenyl-2-propanone, Sulphuric acid, Potassium permanganate na Toluene.

Katika kuhakikisha kwamba kemikali hizi zinasimamiwa na kudhibitiwa, sheria imeainisha taratibu zinazotakiwa kufuatwa kabla ya kemikali hazijaingia nchini au kupelekwa nje ya nchi, na baada ya kuingizwa nchini. Taratibu zilizoanishwa katika sheria hii ni pamoja na kusajili wadau wote wanaohusika na biasahara ya kemikali, kusajili kemikali zote kabla hazijaingizwa nchini, kusajili maeneo yanayohifadhi kemikali, kutoa vibali vya kuingiza na kutoa nje ya nchi kemikali

zote, kutoa vibali vya kusafirisha kemikali ndani ya nchi na kufanya ukaguzi wa kemikali katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za mauzo na matumizi ya kemikali hizo.

Serikali kwa kutumia Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 kwa kushirikiana na taasisi za nje iliweza kuzuia uingizwaji nchini wa kiasi kikubwa cha kemikali bashirifu ambacho hakikuwa na kibali cha kuingizwa nchini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Na. 6: Kemikali bashirifu zilizozuiliwa kuingizwa nchini.**

| AINA YA KEMIKALI | KIASI (Tani) |
|---|---|
| Acetone | 564.00 |
| Hydrochloric acid | 104.95 |
| Methyl ethyl ketone | 100.50 |
| Potassium permanganate | 0.90 |
| Acetic anhydride | 0.04 |
| Sulphuric acid | 100.00 |

Mbali na kuzuia uingizwaji wa kemikali hizo, kuanzia Januari hadi Desemba 2016, Mkemia Mkuu wa Serikali alitoa vibali vya kuingiza kemikali bashirifu kiasi cha lita 653,644,564 kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 7: Orodha ya kemikali bashirifu zilizoingizwa nchini kati ya januari hadi Desemba 2016**

| AINA YA KEMIKALI | KIASI (LITA) | KIASI (Kg) | NCHI ZILIKOTOKEA |
|---|---|---|---|
| Ethyl ether | 92.93 | | India |
| Hydrochloric acid | 114560. 82 | | South Korea, UAE, India |
| Sulphuric acid | 239845. 82 | | South Korea, India |
| Toluene | 299145.00 | | Spain |
| Ephedrine | | 65.56 | Kenya , India |
| Pseudoephedrine | | 973.61 | India, Denmark, Malaysia |

### 3.1.2 Udhibiti wa Dawa za Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa za tiba zenye asili ya kulevya zina umuhimu mkubwa katika kutoa huduma za matibabu kwa wananchi wanaosumbuliwa na maradhi mbalimbali hapa nchini.

Dawa hizi ni pamoja na za kundi la Saikotropiki ambazo zinahusisha Diazepam Lorezepam, Phenobarbitone na nyinginezo. Kundi la pili la dawa hizi ni Nakotiki linalohusisha dawa aina ya Pethidine, Morphine, Etorphine, na nyinginezo.

**Dawa za tiba zenye asili ya kulevya**




Dawa hizi zisipodhibitiwa watu wasio waaminifu huchepusha kutoka katika mfumo rasmi na kuziingiza katika mfumo haramu na hivyo kutumika kama dawa za kulevya. Kwa kutambua hilo, Serikali kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) imeweka utaratibu mzuri wa kudhibiti uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za tiba zenye asili ya kulevya. Aidha, vibali maalum vya uingizaji wa dawa hizo hutolewa kwa makampuni yaliyoidhinishwa kutengeneza na kusambaza dawa za tiba na baadhi ya hospitali hapa nchini.

Katika kipindi cha mwaka 2016 kuanzia Januari hadi Desemba, kwa kuzingatia mahitaji ya nchi TFDA ilitoa jumla ya vibali 58 vya kuingiza nchini dawa za tiba zenye asili ya kulevya kwa waagizaji kutoka makampuni 19. Pamoja na kutoa vibali hivyo katika kudhibiti uchepushwaji, makampuni yaliyopewa vibali vya kuagiza dawa hizo yanawajibika kutoa taaarifa za matumizi ya dawa hizo kila baada ya miezi mitatu. Inapogundulika kuwa dawa hizi zimechepushwa au kuibwa hatua stahiki huchukuliwa dhidi ya wahusika.

**Utoaji wa vibali vya ununuzi wa dawa za tiba zenye asili ya kulevya**

Jumla ya vibali 175 vilitolewa katika hospitali mbalimbali kwa ajili ya ununuzi wa dawa za tiba zenye asili ya kulevya kutoka katika Bohari ya Dawa (MSD) na kuruhusu matumizi ya dawa hizo katika hospitali husika.

**Jedwali Na.8 :Kiasi cha Saikotropiki na tramadol zilizopata kibali cha kuingizwa nchini kati ya mwaka 2014 - 2016:**

| KUNDI LA DAWA | JINA LA DAWA | KIASI KILICHOINGIZWA NCHINI (Kg.) | | |
|---|---|---|---|---|
| Saikotropiki | 1. Diazepam | 93.44 | 24.61 | 45.13 |
| | 2. Lorazepam | 0.32 | 0.30 | 0.66 |
| | 3. Bromazepam | - | 0.01 | 0.46 |
| | 4. Midazolam | - | 0.19 | 0.48 |
| Tramadol | Tramadol Hydrochloride | 408.12 | 162.62 | 222.07 |

### 3.1.3 Kesi za Dawa za Kulevya

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2016 jumla ya kesi 11,054 za dawa za kulevya zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali hapa nchini.Kati ya kesi hizo9,731zilisikilizwa mahakamani ambapo kesi 1,122 zilitolewa hukumu zikihusisha watuhumiwa 21,270.

**Jedwali Na.5.Idadi ya Watuhumiwa naKesi za Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2016**

| AINA YA DAWA | WATUHUMIWA | ZILIZOENDELEA MAHAKAMANI | ZILIZOS-HINDA | ZILIZOS-HINDWA | CHINI YA UPELELEZI |
|---|---|---|---|---|---|
| Bangi | 13,133 | 7,916 | 721 | 184 | 91 |
| Mirungi | 1,755 | 1,254 | 119 | 30 | 62 |
| Cocaine | 194 | 159 | 15 | 4 | 13 |
| Heroin | 528 | 400 | 39 | 10 | 35 |
| Jumla | 15,610 | 9,729 | 894 | 228 | 201 |

### 3.1.4 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya

Mwaka 2016, jumla ya kilo 50 za dawa za kulevya aina ya heroin ziliteketezwa katika kiwanda cha saruji cha Rhino cha Tanga. Uteketezaji wa dawa za kulevya ni suala muhimu katika shughuli za udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya ambao hufanyika kwa utaratibu maalum. Dawa hizi ambazo ni vidhibiti, huteketezwa baada ya kesi kumalizika. Uteketezaji wa dawa za kulevya hufanyika ili; kuzuia uwezekano wa dawa hizo kurudi tena sokoni.

## 3.2 Kinga na Tiba

Serikali ilifanya jitihada mbalimbali katika udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma na huduma za tiba

kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Serikali imeendelea kutoa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya katika vitengo vya afya za akili katika hospitali mbalimbali nchini.

### 3.2.1 Elimu kwa Umma

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2016 makundi mbalimbali ya kijamii yalielimishwa juu ya tatizo la dawa za kulevya kupitia semina, mbio za mwenge wa uhuru, maadhimisho ya kitaifa, vyombo vya habari na machapisho ili waweze kujiepusha na matumizi pamoja na biashara ya dawa za kulevya. Mashirika yasiyo ya kiserikali yalishiriki kutoa elimu kupitia klabu za kupambana na dawa za kulevya kwenye shule za msingi na sekondari, makongamano, matamasha, maigizo na muziki wa injili. Mashirika hayo ni pamoja na T-IOGT, YAVT, AMKUDAKU, CODATZ, Green Hope, Guluka Kwalala, TAYOHAG, NGAO YOUTH GROUP na Changamoto ni Matumaini. Jumla ya wanafunzi 5,232 wa shule za msingi na sekondari, vijana 1,718 na watumiaji wa dawa za Kulevya 492 walipata elimu juu ya madhara yatokanayo na biashara na matumizi ya dawa za kulevya.
Kwa upande wa matukio ya kitaifa, elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa katika Maadhimisho ya Wiki ya Vijana Kitaifa, Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru na Kumbukumbu ya Kifo cha Baba wa Taifa mkoani Simiyu. Vyombo vya habari vilishiriki katika kuhabarisha umma kuhusu tatizo la dawa za kulevya ambapo Taarifa kwa umma ilitolewa ikiainisha ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya, sheria ya kudhibiti tatizo la dawa za kulevya, ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa hizo na udhibiti wa mali zinazopatikana kwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya kwa vyombo mbalimbali vya habari kupitia Idara ya Habari Maelezo.

Ujumbe juu ya madhara yatokanayo na dawa za kulevya uliingizwa katika kitabu cha mbio za mwenge wa uhuru na kusambazwa nchi nzima, ujumbe huu ulielezea ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya. Pia taarifa ya hali ya dawa za kulevya, vipeperushi vinavyoelezea madhara ya dawa za kulevyana mabango vilisambazwa nchi nzima.

### 3.2.2 Tiba ya Methadone

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo iliendelea kutoa tiba maalum kwa waathirika wa dawa ya kulevya aina ya heroin ambapo hadi 2016 kulikuwa na jumla ya kliniki tatu zilizopo katika hospitali ya taifa ya Muhimbili, Mwananyamala na Temeke.

Katika kliniki hizo waathirika wa dawa za kulevya hupewa dawa aina ya methadone kwa ajili ya kuwazuia kupata hamu ya matumizi ya dawa ya heroin na dawa nyingine za kulevya. Huduma hii pia inatoa fursa kwa waathirika wa dawa

za kulevya kuweza kupata huduma zingine za afya kama vile; kupima Virusi Vya UKIMWI, kupata dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, tiba za kifua kikuu, magonjwa ya zinaa, homa ya ini aina B na C na magonjwa ya akili.

**Waathirika wa Dawa za Kulevya katika Kliniki za Methadone.**
Yafuatayo ni majedwali yanayoonesha takwimu za waathirika wa dawa za kulevya wanaopata huduma za tiba ya methadone katika kliniki za Mwanayamala, Temeke na Muhimbili katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2016.

**Jedwali Na. 9: Kliniki ya Methadone Mwananyamala**

| | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|
| Jumla ya walioandikishwa | 1,167 | 203 | 1,370 |
| Waliobaki kwenye Tiba | 849 | 143 | 992 |
| Walioacha | 225 | 35 | 260 |
| Maambukizi ya VVU | 152 | 76 | 228 |
| Wagonjwa wa Kifua Kikuu | 58 | 26 | 84 |

**Jedwali Na. 10: Kliniki ya Methadone Muhimbili**

| | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|
| Jumla ya walioandikishwa | 1,201 | 77 | 1,278 |
| Waliobaki kwenye Tiba | 849 | 59 | 943 |
| Walioacha | 183 | 18 | 201 |
| Maambukizi ya VVU | 241 | 28 | 269 |
| Wagonjwa wa Kifua Kikuu | 82 | 16 | 98 |

**Jedwali Na. 11: Kliniki ya Methadone Temeke**

| | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|
| Jumla ya walioandikishwa | 857 | 48 | 905 |
| Waliobaki kwenye Tiba | 589 | 29 | 618 |
| Walioacha | 188 | 17 | 205 |
| Maambukizi ya VVU | 152 | 18 | 160 |
| Wagonjwa wa Kifua Kikuu | 37 | 9 | 46 |

Hadi kufikia mwezi Disemba 2016, kliniki ya Methadone katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambayo ilianzishwa rasmi tarehe 4 Februari 2011 ilikuwa na jumla

ya wagonjwa 1,278. Kwa upande wa kliniki ya Methadone katika hospitali ya Temeke ambayo ilianzishwa tarehe 28 Machi 2014 idadi ya wagonjwa ilifikia 905, kwa hospitali ya Mwananyamala ambayo ilianzishwa tarehe 6 Novemba 2012 idadi ya wagonjwa ilikuwa 1,370. Jumla ya wagonjwa 3,553 wenye umri kati ya miaka 15-63 walipata huduma za methadone katika kipindi hicho. Kati yao wagonjwa 943 walihudhuria vizuri na kupata tiba kwa ufasaha katika hospitali ya Muhimbili, wakati hospitali ya Temeke 618 na Mwananyamala ni 992.

Faida za tiba ya Methadone ni pamoja na; kupunguza matumizi ya dawa za kulevya nchini, kupungua kwa vitendo vya kihalifu katika jamii, kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI na magonjwa mengine yanayoambukizwa kwa njia ya damu kwa watumiaji wa dawa za kulevya hasa kwa kujidunga na hatimaye kuenea katika jamii yote kwa ujumla, kuboresha afya za waathirika wa dawa za kulevya na maisha yao kwa ujumla na kupunguza vifo vitokanavyo na madhara ya dawa za kulevya. Pia, Huduma hii inatoa fursa kwa waathirika wa dawa za kulevya kuweza kupata huduma nyingine za afya kwa kufanyiwa vipimo na tiba za kifua kikuu, homa ya ini, magonjwa ya akili na kupunguza uwezekano wa kuenea kwa kifua kikuu sugu na  uwezekano wa kuenea kwa usugu wa tiba za dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI. Huduma hii inapunguza unyanyapaa kwa waathirika wa dawa za kulevya katika jamii na kurudisha mahusiano mazuri na ndugu, jamaa na marafiki na jamii kwa ujumla. Afya za watumiaji wengi wa dawa za kulevya zimeimarika na wengi wameweza kufanya shughuli mbalimbali za kuweza kuwaingizia kipato.

Pamoja na hilo jitihada mbalimbali zinafanyika kwa ajili ya kuanzisha vituo vingine kama hivyo katika mikoa iliyoathirika zaidi na matumizi ya heroin kama vile Mbeya, Mwanza, Dodoma, Arusha na Tanga.

**Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)**

Nyumba za upataji nafuu hutoa huduma kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa kutumia hatua kumi na mbili (12) za upataji nafuu, ambapo mtumiaji wa dawa za kulevya hukaa katika nyumba ya upataji nafuu kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Nyumba hizo hufundisha namna ya kuishi bila kutumia dawa za kulevya na stadi mbali mbali za maisha atakazozitumia baada ya kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile ushonaji, upishi, uchongaji wa vinyago na usafi.

Huduma hizi za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya zimekuwa zikianzishwa na  mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambapo kwa mwaka 2016 nyumba hizo ziliendelea kufunguliwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ikiwemo Dar es salaam, Pwani, Tanga, Iringa, Mwanza Kilimanjaro na Tabora.

**Jedwali Na. 12: Mashirika yaliyoanzisha Nyumba za Upataji Nafuu**

| Na. | Mkoa | Shirika lisilo la Kiserikali |
|---|---|---|
| 1 | Dodoma | PEDDEREF |
| 2 | Dar es salaam | Pilimisanah Foundation |
| | | PEDDEREF |
| | | Changamoto ni Matumaini |
| | | Imani Recovery and Sobriety care center |
| | | Drug free Tanzania |
| | | South beach sober house |
| | | Right way recovery house |
| | | The Coin Foundation |
| 3 | Pwani | Life and Hope Rehabilitation Organization |
| | | Filberty Bayi Foundation |
| 4 | Tabora | Tabora sober house |
| 5 | Tanga | Tanga Drug Free |
| | | Gift of Hope Foundation |
| 6 | Iringa | Iringa sober house |
| 7 | Kilimanjaro | Kilimanjaro new vision |
| | | Kipepeo foundation |
| 8 | Mwanza | Pilimisanah Foundation |

**Jedwali Na.13: Idadi ya waathirika wa dawa za kulevya walipatiwa huduma kwenye nyumba za upataji nafuu (sober house).**

| Shirika | Waliojiunga | Walioshindwa kumaliza programu | Waliorudia matumizi | Waliomaliza Programu |
|---|---|---|---|---|
| PEDDEREF | 167 | 9 | 25 | 125 |
| Imani Recovery and Sobriety care centre | 40 | 22 | 14 | 4 |
| Gift and Hope Foundation | 36 | 17 | 8 | 9 |
| Drug Free Tanzania | 104 | 40 | 26 | 38 |
| South beach sober house | 156 | 50 | 66 | 106 |
| Right way Recovery house | 42 | 12 | 12 | 30 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Tanga Drug Free No. 1 | 80 | 28 | 12 | 52 |
| Tanga Drug Free No. 2 | 73 | 31 | 18 | 24 |
| Daytop Preventive Drugs Dependence Foundation | 60 | 2 | | 58 |
| Tabora Sober House | 10 | 4 | 1 | 5 |
| Changamoto ni Matumaini | 99 | - | - | 19 |
| Kilimanjaro New Vision | 135 | - | - | 43 |

# SURA YA NNE

## 4 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE

### 4.1 Changamoto

1) Ufinyu wa rasilimali fedha na rasilimali watu,

2) Ukubwa wa Mipaka wenye vipenyo vingi visivyo rasmi pamoja na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi hufanya udhibiti wa dawa za kulevya kuwa ngumu,

3) Uelewa mdogo juu ya madhara ya dawa za kulevya na njia sahihi za kupambana na tatizo hilo miongoni mwa wananchi,

4) Kubadilika mara kwa mara kwa mbinu za ufungaji na usafirishaji wa dawa za kulevya kunakofanywa na wafanyabiashara wa dawa hizo,

5) Kilimo cha Bangi na Mirungi kufanyika maeneo ya milima na misitu minene isiyofikika kirahisi,

6) Uhaba vya vifaa vya kisasa vya kugundua dawa zinapoingizwa au kusafirishwa ndani ya nchi na kugundua mashamba ya bangi na mirungi kama vile setelaiti, helikopta na boti,

7) Watumiaji wa dawa za kulevya kuwa na maambukizi ya magonjwa mbalimbali yanayoweza kusambaa kwenye jamii hasa VVU/ UKIMWI, Kifua kikuu sugu na homa ya ini,

8) Ukosefu wa vituo vya kujengea uwezo wa ujasiliamali wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya ili aweze kujitegemea na kuachana kabisa na mtumizi ya dawaza kulevya,

9) Utofauti wa ukali wa sheria ya kudhibiti na kupambana dawa za kulevya katika nchi tunazopakana nazo, hivyo kusababisha wafanyabiashara kufanya shughuli zao kutokea nchi zenye sheria laini.

## 4.2 Hatua za Kukabiliana na Changamoto

1) Kuwapatia mafunzo watumishi wa Mamlaka ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo

2) Suala la dawa za kulevya kuwa Agenda ya kudumu kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa na wilaya zote nchini

3) Kuendelea kuanziasha klabu za mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika shule zote za msingi na sekondari nchini.

4) Kuongeza vituo vya matibabu ya Uraibu hasa katika mikoa iliyoathirika zaidi na tatizo la matumizi ya dawa za kulevya.

5) Kujenga Kituo kitakacho jihusisha na kutoa elimu ya ujasiriamali pamoja na mafunzo ya ufundi kwa waraibu walio achakutumia dawa za kulevya.

6) Kuwa na vifaa vya kisasa ili kurahisisha utambuzi wa dawa za kulevya zinaposafirishwa na wafanyabiashara wa dawa hizo na utambuzi wamashamba ya bangi na mirungi

7) Kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki mapambano dhidi ya dawa za kulevya kama vile maofisa forodha wa mipakani, bandarini na viwanja vya ndege, vyombo vya ulinzi na usalama na waendesha mashtaka ili waweze kuongeza ufanisi katika udhibiti wa dawa za kulevya.

8) Kuanzisha maabara ya sayansi jinai itakayosaidia kutambua aina mbalimbali za dawa za kulevya zilizokamatwa pamoja na kubaini watumiaji wa dawa hizo